# SUNNAH NA HADITHI

# FORM ONE

Maswali ya wakati wa likizo

Maelekezo:

Nakili maswali yote kisha pigia msitari katika sentensi sahihi tu.

**Maana ya Sunnah na Hadithi-01**

1. **Mwenendo au mila yoyote kilugha huitwa:**

   **Sunnah**

   **Hadithi**

   **Tawhiid**

   **Tarekh**

2. **Neno Sunnah kiutendaji huskughulika na**

   **Matendo ya msingi aliyoyafanya Mtume saw**

   **Matendo ya kiutamaduni aliyofanya Mtume saw**

   **Matendo ya kiuchumi tu aliyofanya Mtume saw**

   **Matendo ya kiustaarabu tu aliyofanya Mtume saw**

3. **Swalini kama mlivyoniona nikiswali huu ni mfano wa**

   **Hadithi katika matendo**

   **Hadithi katika maneno**

   **Hadithi katika kauli**

   **Hadithi katika vitendo**

4. **Mtume saw alimruhusu swahaba kusoma suratul ikhlas katika kila rakaa hii nihadithi inayoonesha**

   **Kukubali matendo ya swahaba**

   **Kumtukuza swahaba**

   **Kumuonea wivu swahaba**

   **Kukubali unadhifu wa swahaba husika**

5. **Masimulizi ya matendo ya Mtume saw kwa kifupi huitwa**

Sunnah

Bid-aa

Khurafii

Answar sunnah

6. Hadithi nabawiy zina sifa ya kuwa

Masimulizi na ujumbe vyote hutoka kwa Mtume saw

Masimulizi hutoka kwa Mtume Ujumbe hutoka kwa Allah

Zote sipo sawa

Hadithi ypypte imetoka kwa Mtume saw

7. Sifa kuu ya Hadithil qudusy ndani yake utalikuta tamko

Mutafakun illaihi

Rawahu shsikhan

Rarahu Tirmiddhi

Allah Amesema

8. Hadithi zote zinaonesha kuwa :

Muhammad ni mtume wa kweli

Muhammad hatamki kwa matamaniyo

Muhammad ni baba wa Mitume wote

Muhammad ni muotaji Hodari wa mambo ya ghaibu

9. Zifuatazo ni kazi za Mtume saw kutokana na aya 3:164 isipokuwa

Kuwafundisha watu

Kufundisha heima

Kufundisha njia salama

Kuwaonesha watu pete za bahati

10. Amesema bibi Aisha r.a Mtume saw alikuwa akisali swala ya dhuha rakaa nne na mara nyingine alikuwa akizidisha atakazo. Huu ni mfano wa hadithi katika

Maneno

Vitendo

Kukiri

Kuridhia

Kazi ya Sunnah na hadithi-02

1. Kazi ya sunnah na hadithi kuendana kwa mujibu wa Qurani ni:

Kutoa ufafanuzi wa mwisho juu ya ayah

Kujazilishia aya zenye mapungufu

Kutaja herufi zilizomo ndani ya Ayah

Kutoa uhalisia wa mambo ya ghaibu tu kwa wataalamu wa elimu ya ghaibu

2. Namna ya utekelezaji wa ibada mbalimbali unapatikana kwa

Uzoefu kwa kuwaangalia wazazi wetu ambao ni waislamu

Kuangalia mashekhe wakubwa wakubwa namna wanavyofanya ibada zao

Maelekezo yanatokana na hadithi na sunnah

Maelekezo na ufafanuzi kutoka kwa wanawachuoni na maoni yao binafsi tu.

3. Moja ya kazi za hadithi zinazohusiana na sifa za Mtume saw zinatufahamisha kuwa:

Tuzijue sifa za mtume saw na kumsifia sana kwa sifa hizo

Tuige mwenendo wake ambazo ni sifa njema zaidi

Tumtukuze sana mpaka hata wasio waislamu wamjue bwana wa viumbe

Tumlinganishe na mitume wengine ili tuone ubora wake juu yao

4. Sunnah na hadithi huchukua nafasi ya ……. Katika sheria za kiislamu

Kwanza

Pili

Tatu

Nne

5. Kutokana na Qurani 3:32 Tunahimizwa kuntii Allah na Mtume wake ili tupate…

Thawabu nyingi

Kurehemewa

Kutajirishwa

Kuwa Maarufu duniani na Akhera.

6. Kutokana na Sura 4:59 inawataka waumini wakitatizwa na jambo wafanye nini ?

Watafute hakimu ahukum baina yao

Warudi kwa Allah na Mtume saw

**Waende wakatumie fursa walizonazo mtaani**

**Wapambane kuhakikisha hilo jambo linaondoka kwa akili zao wenyewe**

7. **Sura ya 5:92 inawatak waislamu wajikinge na:**

   **Mangonjwa ya kuambukizwa kama korona**

   **Kukhalifu amri za Mtume saw**

   **Kukhalifu amri za viongozi wao wa ngazi ya juu**

   **Kwenda hovyo bila ya kuzingatia maslahi yao.**

8. **Kwa mujibu Qurani 24:54 kazi ya Mtume saw iliyotajwa kwa umma ni:**

   **Kuhakikisha umma wote unafuta dini ya Allah**

   **Kufikisha tu ujumbe wa Allah**

   **Kuhakikisha kila kitu kinaenda vizuri katika uchumi**

   **Kuhakikisha kila mjane na yatima anapata haki zake**

9. **Matokeo yanayotajwa katika 47:33 ya kutotii Amri za Allah na Mtume wake ni:**

   **Kuharibika amali za mja**

   **Kukosekana thawabu za kutosha kwa mja**

   **Kulipwa kidogo kwa mja**

   **Kukosekana umoja miongoni mwa waje**

10. **Watu wema kwa mujibu wa qurani 3:68 ni wale waliofuata …… na nabii huyu Muhammad saw**

**Yunus as**

**Ibrahim as**

**Hud as**

**Yusuf as**

**Uandishi wa Hadithi -03**

1. **Moja ya sababu zifuatazo zilisababisha uandishi wa hadithi kuwa hafifu wakati wa Mtume saw isipokuwa moja tu nayo ni:**
   **Mtume hakujua kusoma na kuandika**
   **Mtume alikuwepo hivyo kazi ilikuwa ni kumuiga tu**
   **Walikatazwa mwanzoni kuandika walivyoruhusiwa wakawa wamezoea kutoandika**
   **Walihofia kuchanganya hadithi na Qurani**

2. **Nyenzo pekee iliyotumika kuhifadhi hadithi wakati wa Mtume saw ni**
   **Vifua vya maswahaba na matendo yao**
   **Mawe na Ngozi zilizohifadhiwa**
   **Vitabu kama Bukhari na Muslim**
   **Vitabu vya hadithi maarufu kama Bayhaqy.**

3. **Moja ya wanawake waliohifadhi hadithi nyingi Zaidi alikuwa anaitwa:**
   **Hafsa bint umar mke wa Mtume saw**
   **Aisha bint abu bakri**
   **Khaula bint Thaalabah**
   **Hindu bint Utbah**

**4. Anaeongoza kwa wingi wa Hadithi za Mtume saw katika uhifadhi kwa wanaume alikuwa ni:**

**Hamza bin Abu-twalib r.a**

**Abuu said alkhudhriyy r.a**

**Thaalabah bin Hatiim r.a**

**Abu Huraira r.a**

**5. Hatua ya pili ya uandishi wa Hadithi za Mtume saw ni :**

**Karne ya Kwanza Hijiria**

**Karne ya pili hijiria**

**Karne ya tatu hijiria**

**Karne ya nne hijiria**

**6. Swahaba wa mwisho kutawafu kutokana na riwaya nyingi aliitwa:**

**Abu tufayl Amir Alwathillah r.a**

**Amru bin Ummaya r.a**

**Anas Bin Malik r.a**

**Amru bin al- As r.a**

**7. Moja ya changamoto zilizosababisha ikaonekana umuhimu wa hadithi na sunnah wakati wa maswahaba ni:**

**Swali Mtume aoshwe nan ani**

**Swali mtume azikwe wapi**

**Swali Mtume aswaliwe nan ani**

**Swali Nani awe kiongozi wa dola**

8. **Al-qatadaya ipo sambamba kabisa na safu ipi ya kitabu cha hadithi**
   **Swahihi Bukhari**
   **Swahihi Muslim**
   **Juzuu ya Ibn Hambal**
   **Juzuu ya Ibn Abbas**

9. **Aliekusanya Mashekhe wa mwanzo kabisa ili waanze kuhakiki hadithi baada ya ugomvi wa kisiasa baina ya umma wa kiislamu ni:**
   **Umar Mukhtar**
   **Umar bin Abdul aziz**
   **Tabiina Musab bin khashtar**
   **Abu Ubaydah amir al-jarah**
10. **Moja kati ya hawa mashekhe alisimamia kazi ya kuhakiki hadithi wa mwanzo kabisa**
   **Muhammad ibn Shihab (Al zubery)**
   **Muhammad ibn Yuusu (Al-yaman)**
   **Muhammad ibn Khardhwawi (al-misryy)**
   **Muhammad ibn Jamal (al-farsy)**

**Uandishi wa Hadithi -04**

1. **Watu waliwaona maswahaba na wakawaamini na kuwa waislamu na wakafa wakiwa waislamu huitwa:**
   **Maulammaa**
   **Wanawachuoni**
   **Tabiina**

**Tabii Tabiina**

2. **Uandishi wa Hadithi hatua ya tatu ulikuwa katika kipindi cha:**
   **101 – 200H**
   **201 – 300H**
   **301 – 400H**
   **401 – 500H**

3. **Orodha ifuatayo ni ya Muhadithina waliotokea katika wakati wa Tabiina isipokuwa**
   **Ma'amar bin Rashid**
   **Abdulmalik bin Juraij**
   **Sufiyan bin Uyaina**
   **Miqdaad bin Aus**

4. **Wakati ambao zilianzishwa vituo mbalimbali vya mafunzo ya hadithi (learning centres) pamoja na umoja wa watu wa hadithi muhadithina ni:**
   **Karne ya kwanza Hijiria**
   **Karne ya pili hijiria**
   **Karne ya tatu hijiria**
   **Karne ya nne hijiria**

5. **Imam Malik bin Anas alieishi madina kati ya 95H na 179H alijulikana Zaidi kwa kitabu chake kilichokuwa katika kipindi cha tabiina kilichoitwa:**
   **Al-musnad**

**Al-muwatta**

**Al-dirhamy**

**Al-Qasas -l haqq**

6. **Moingani mwa sababu za Tabii Tabiina kuendeleza uandishi wa hadithi baada ya kuwepo Al-muwatta ilikua ni pamoja na :**

   **Upataikanaji wake ulikuwa ni huko Hijaz tu na kugusia ibada maalum tu**

   **Gharama zake zilikua za juu sana**

   **Kilipatikana kwa lugha moja tu**

   **Kilikua na baadhi ya alama za ubaguzi kwa baadhi ya watu**

7. **Sahihu sita zilikusanywa katika kipindi cha:**

   **Mtume saw**

   **Maswahaba ra (karne ya kwanza)**

   **Tabiina (Karne ya pili)**

   **Tabii Tabiina (Karne ya tatu)**

8. **Kilele cha uandishi wa hadithi kilikuwa katika…**

   **Karne ya nne**

   **Karne ya tatu**

   **Karne ya pili**

   **Karne ya kwanza**

9. **Miongoni mwa vitabu vilivyoandikwa na kuwa maarufu mbali na sahihu sitta ni :**

**Kitabu cha Al-waqidi**

**Sunan ya Ann-nasai**

**Sunan ya ibn majah**

**Al-jamiu ya Tirmidhi**

10. **Kitabu cha mwisho kilichoandikwa baada yah apo tu ndio zikaja sahihu sita ni:**

    **Sunan ya Darimi**

    **Kitabu cha Bayhaqi**

    **Kitabu cha Ibn Qudama**

    **Kitabu cha Ibn Munthir**

Kuhifadhiwa Hadithi -05

1. **Zana kuu ya kuhifadhi hadithi wakati wa Mtume saw ilikuwa ni :**

   **Vifua vya maswahaba na Maandishi kwa uchache**

   **Maulamaa wakati wa Mtume**

   **Ngozi na mawe**

   **Makuti na Vifaa vya wakati huo**

2. **Maimamu wa zama za kati aliefanya hadithi kuwa fani maalum katika uislamu ni:**

   **Imamu Bukhari**

   **Imamu Suyut**

   **Imam Ibn hajar Asqalaani**

   **Imam Nawawiy**

**3. Orodha ifuatayo ni ya waandishi wa hadithi wakati wa Mtume saw isipokuwa**

**Rafii bin Khariij**

**Jaabir bin Abdillah**

**Abdillah bin Abi Auf**

**Al-hassan Albassary**

**4. Ni mkusanyaji wa hadithi, au mwandishi wa hadithi katika kitabu, mara nyingi ni mtu wa mwanzo kutajwa au wa mwisho katika hadithi yoyote**

**Rawi**

**Bukhari na Muslim**

**Abu Huraira**

**Ibn Abbas**

**5. Ni yale maneno yenyewe hasa aliyoyasema Mtume saw, au maelekezo ya sahaba alivyomuona mtume saw akitenda jambo Fulani.**

**Sanadi**

**Isnadi**

**Naswu au Matini**

**Al-musnad**

**6. Hadithi imepokelewa na imamu *Malik bin Anas* katka Kitabu chake Al-muwatta ambae kaipokea kutoka kwa *Nafii* ambae nae kapokea kutoka kwa *Abidillah bin Umar* alimsikia Mtume saw**

**akisema *Kila jambo jema analolifanya mwislamu ni swadaka*,**

**Isnadi katika hadithi hii ni:**

**Imamu Maliki**

**Nafii**

**Abdillah bin Umar**

**Imam Malik, Nafii, Abdullah bin Umar**

7. **Ni kumtia ila mbaya msimuliaji kwa kuikataa hadithi yake kutokana na udhaifu au kasoro alizokuwa nao, hii huitwa:**

   **Al-jarhi**

   **At-taadili**

   **Rahbatil- hadith**

   **Asmaaul-rijal**

8. **Ni hadithi yenye matini moja au matini yenye maana moja lakini imesimuliwa na mtiririko wa watu zaidi ya mmoja**

   **Riwaya**

   **Hekaya**

   **Mutafakun alaihi**

   **Rawahu shaikhani**

9. **Ili Isnadi ikubalike moja kwa moja kuwa ni sahihi ni lazima:**

   **Hakuna seheme ilipokatika (hakuna nafasi iliyoachwa kati ya wasimuliaji wake wote)**

   **Iwe imetolewa na Mtu kabila la kiarabu**

   **Iwe imeletwa kwa mwandishi wakati wa Mtume saw**

**Iwe ndani yake imetaja sifa za Mtume saw**

**10. Katika uchunguzi wa Matini yafuatayo huangaliwa isipokuwa moja tu nalo ni :**

**Isiende kinyume na Qurani**

**Isigongane na hadithi nyingine sahihi iliyosadikishwa kwamba ni sahihi**

**Isiende kinyume na Ukweli wa kihistoria halisi uliopo**

**Isiende kinyume na ukweli wa mambo yaliyosimuliwa na watu wanaofahamika**